



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Wednesday, 11th March, 2025

Third Assembly – Fourth Session
NINETH SITTING

*[The County Assembly met at 10:20a.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Members you may be seated. Yes Clerk?

COMMUNICATION FROM THE CHAIR
STUDY VISIT – BRIJAM INTEGRATED ACADEMY

Honourable Members, the County Assembly is privileged to welcome students and teachers from Brijam Integrated Academy from Kisauni Constituency.

Hon. Kai: They are from Kisauni Constituency, Junda Ward.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay, thank you Honourable Sylvester Kai he has confirmed that the students are from Junda Ward, Kisauni Constituency. I will name the names of the students and the teachers present so please when you hear your name just stand up and bow.

1. Briggs Edgeland
2. Abigail Kerubo
3. Saumu Amir
4. Edith Oyo
5. Jefwa Omweri
6. Abigail Nyiro
7. Lillian Sidi
8. Amina Gira
9. Samuel Ondiek
10. Emanuel Andi
11. Emanuel Shukurani
12. Rajab Gira
13. Beatrice Mluo

14. Collins Gamble
15. Anita Maria
16. Joy Njeri

Accompanied by their teachers;

Mr. Joseph Ochieng

1. Mr. Victor Odhiambo
2. Mr. Kenneth Kinuthia
3. Mr. Job Oko
4. Ms. Sakina

Welcome once again to the County Assembly of Mombasa and I will let...

[Applause]

2. Honourable Members to say a word, starting with a Member from Junda Ward and the Leader of the Majority Party, thank you.

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Kwanza nichukue hii fursa kuwakaribisha wanafunzi wa Brijam Integrated pamoja na waalimu katika Jumba hili ikiwa wameweza kutembea sehemu hii kama sehemu ya masomo niwaambie mujisikie muko nyumbani na mumekaribishwa sana na uongozi wote wa Bunge. Mheshimiwa Spika, hizi ni kati ya zile shule ambazo zinapatikana ndani ya Junda na hii inaonyesha mfano mzuri wa kwamba usimamizi wa shule hii inanuia kuhakikisha ya kwamba inawapatia watoto masomo Ikingatiwa kwa sasa hivi ni masomo ya mfumo wa Competence Based Curriculum, CBC inategemea pakubwa sana kwa kuona. Kwa hivyo wanafunzi niwahimiza ya kwamba mchukue fursa hii kuelewa mengi hata baada ya hapa najua mutaweza kuonyeshwa ni jinsi gani shughuli za Bunge zinaendeshwa. Na naamini wengine mutaweza kupata motisha ya kwamba badala ya Mheshimiwa Kai baadae atakapo panda ngazi kubwa za uongozi na najua wengine wenu pia vile vile mutaweza kua Waheshimiwa na muongoze Junda vizuri kama vile Mheshimiwa Sylvester Kai anaendeleza Junda. Na mumeiona inaendelea vizuri na kwa sababu mumetembea hapa, nataka niwahakikishie ya kwamba nitatembea niangalie ile barabara yaelekea kwa shule yenu ili hapa mbeleni ninapopata barabara nihakikishe ya kwamba shule yenu imeweza kuwa na njia nzuri ili wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri. Lakini nichukue fursa hii kumpatia salamu za kipekee Lilian Sidi kwa sababu ni somo ya mke wangu kipenzi kwa hivyo niseme ya kwamba nitamuona baada ya hapa. Ahsante sana na Mungu awabariki...

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Leader of Majority Party?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali ya yote kwanza nikaribishe wanafunzi wetu na walimu kwa kua hapa kwa ziara ya kimasomo kuhusiana na swala zima la ugatuzi. Mheshimiwa Spika, ugatuzi umetokana na sura ya 11 ya Katiba yetu ya Kenya, hio ndio ilizalisha unapoisoma sehemu yake pili, sehemu ya kwanza inazungumzia maudhui na kanuni za utatuzi, sehemu yake ya pili ya sura hio inazungumzia vitengo vya ugatuzi ambacho kitengo cha kwanza ni Bunge la Kaunti halafu pili ndio ni utawala wa Kaunti.

Kwa hivyo hili ni muhimu kwa wanafunzi wetu ya kwamba hili swala ambalo wamekuja jifunza lipo ama limeangaziwa katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Kenya sura ya 11, ama chapta 11 kawa watatizika. Vile vile Mheshimiwa Spika, imedukuu Katiba hio inapokwenda ratiba...

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): ...Imedukuu Katiba hii unapokwenda ratiba ya 4 (2) kuangazia majukumu yetu sisi kama Bunge ama kama Gatuzi. Sehemu (1) ya ratiba ni majukumu ya Serikali ya Kitaifa, sehemu (2) ni majukumu ya Serikali Gatuzi ambayo tumepewa majukumu 14 Mheshimiwa Spika ambayo ni wajibu wetu sisi kama Gatuzi kuweza kuyaangazia. Lakini cha msingi Mheshimiwa Spika unapokwenda katika County Government Act ama sheria za Ugatuzi ambao ni sheria ya Bunge ambayo ya mwaka 2012 inapeana taratibu za shughuli za Bunge, shughuli za kila Mheshimiwa na shughuli za ofisi ya utawala ikiongozwa na Mstahiki Gavana. Moja wapo ya majukumu Mheshimiwa Spika sisi kama wawakilishi hatutekelezi majukumu ya ki utawala, kwa hivyo Mheshimiwa mwenza ambao wanafunzi wanatoka kwake amewapa ahadi ya kwamba akipata barabara atawapelekea. Lakini ni jukumu lake kupigania barabara kwa bajeti iwekwe ili iende sio yeye kuipeleka kwa sababu si jukumu lake la utekelezaji; isije ikanukuliwa vibaya ya kwamba Waheshimiwa wanajenga barabara Mheshimiwa sisi hatutekelezi kwa mujibu wa sheria yeye apambane...

[Interruption]

Hon. Kai: Naona Kiongozi wa Wengi ama Kiongozi wa Bunge yuko sahihi lakini pia nataka niweke wazi ya kwamba mimi kama Mheshimiwa wa Junda ninafahamu sana ya kwamba mimi sio mtekelezaji lakini hawa wananchi wa Junda walinituma kuzungumza kwa niaba yao. Kwa hivyo ninaposema kwamba nitapeleka barabara ni kwamba hakutatoka mwananchi wa Junda aje apitishie bajeti hapa isipokua ni mwakilishi wao hivyo nina maanisha sawia na unachosema ya kwamba nitapitisha bajeti ambayo itawasaidia kupata barabara. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa nimshukuru Mheshimiwa kwa kuliweka wazi kwa sababu mwengine hua kuna shughuli za Bunge zikiendelea tuko na vyombo vya habari, tuko na mitandao ambayo inaangazia moja kwa moja. Nisingetaka ndugu yangu anukuliwe ya kwamba amechukua dhamana ambalo si lake; lakini ameiweka bayana. Hayo ni katika yale majukumu na sisi kama Bunge kwa sababu ameashiria barabara hii inaelekea kwa ajili ya kuboresha maeneo ya watoto wetu watakayosoma sisi kama Bunge tutamuunga mkono katika bajeti tuhakikishe ya kwamba barabara yake imeweza kuangaziwa kwa ajili ya wanafunzi lakini zaidi watu wa Junda. Ahsante Mheshimiwa Spika na nawakaribisha tena wanafunzi wetu, shukran Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you, Leader of Majority. Yes, Clerk next order please?

MOTION

NAMING A ROAD IN HONOUR OF THE LATE MR. HASMUKH PATEL KANJI

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Members, I was notified that Honourable Ibrahim Omondi was the one to move this Motion, so Honourable Ibrahim Omondi proceed.

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker. I can confirm that it is indeed true that we had a conversation with the Member of Tudor Ward who was actually run this particular Motion and we agreed that I will do no his behalf. Naming a road in Honour of the Late Mr. Hasmukh Patel Kanji commonly known as Mombasa Cement. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion,

THAT AWARE that the Fourth Schedule, Part 2, Section 5, (a) of the Constitution of Kenya, 2010 assigns County Government the role of managing County transport including County;

NOTING THAT Mr. Hasmukh Patel Kanji was a prominent philanthropist in Mombasa who contributed immensely to the welfare of the community through numerous charitable initiatives including feeding programs, educational scholarships, support for persons with disability and the transformation the Kibarani dump site into a recreational park.

ACKNOWLEDGING the indelible impact of Mr. Patel's charitable actions, which continue to uplift the residents of Mombasa, thus embodying an inspiring model of selfless service and dedication to communal welfare; Mr. Speaker, sorry Mr. Speaker of late I have been having problems with my eyes but I think I will visit a specialists to be able to...

RECOGNIZING the need to honour such an exemplary individual whose contributions resonate deeply within the community, therefore setting a benchmark for social responsibility and public service;

CONCERNED that the failure to acknowledge such a significant contributor to the community would overlook an important figure in Mombasa's recent history;

I, therefore urge this Assembly to RESOLVE:

That the County Government of Mombasa, through the Department of Transport and Infrastructure, formally designate and name a road as, "Hasmukh Patel Kanji Road" in perpetual honour of the late Mr. Hasmukh Patel Kanji's invaluable contributions to the County and his enduring legacy of community service.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Who is your seconder?

Hon. Omondi: I beg Honourable *Letarazi* to second.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Who is Honourable *Letarazi*? We do not have a Honourable Member by that name, Honourable Ibrahim!

Hon. Omondi: Honourable Juma Mwalimu, commonly known as *Letarazi*.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Juma Mwalimu?

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Mswada huu.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now propose a question that the Motion as moved by Honourable Ibrahim Omondi on Naming of a road in honour of the late Hasmukh Patel Kanji be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Ibrahim Omondi?

Hon. Omondi: Yes Mr. Speaker, Mr. Speaker it is....

[Interruption]

Hon. Omondi: Yes Mr. Speaker, it is indeed true that what we are doing today is our legal mandate; we all know we cannot actually hide our heads under the sun and pretend that we do not know the contribution that Honourable Patel made to our community especially Mombasa County as a whole. Mr. Speaker, the fact that he is not there this still remains in our memories that Mr. Patel has done a lot, he has contributed a lot in our community in terms of welfare, in terms of distribution of water to our Wards, to our County, the biggest of all is when he managed to change the Kibarani dumpsite into a very nice place. Mr. Speaker, it will only be right that today as Members of the County Assembly of this particular Honourable House that will do justice and i do not think if there is any Member who will oppose, a Motion runs down my head when I remember the immense contribution that Mr. Patel contributed to our community. Mr. Speaker, this will be the only way by which we shall remember him by naming a road after him; therefore, I want to urge the House that we all agree that this Motion is important and we all pass it. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Juma Mwalimu?

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono Mswada huu ulioletwa na ndugu yetu kutoka pale Tudor, na si uongo marehemu aliweza kusaidia kwa hali na mali yake na wakaazi wa Mombasa wengi na viunga vyake wameweza kufaidika na msaada wake sio mahospitali, sio mashule na hata vyakula pia kwa hiyo kutajwa jina lake kwa barabara ni haki yake. Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Jacktone Madialo?

Hon. Madialo: Thank you Honourable Speaker for the opportunity. Honourable Speaker, the late Mr. Hasmukh Patel Kanji was an industrialist whose main flagship industry was constituted in my Ward so for that and many reasons I support.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Honourable Joshua Ong'au?

Hon. Ong'au: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ili na mimi pia niweze kuchangia Hoja ambayo iko kwa Nyumba leo. Kwa kweli ambaye tunamzungumzia Patel Kanji aliweza kusaidia jamii sana kwa hivyo naunga mkono barabara iweze kuitwa jina lake.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Kachumbo Florence?

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity like my colleague have said the late Patel was quite a generous man and he helped millions of people so I stand to support the Motion.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Honourable Kai Sylvester?

Hon. Kai: Ahsante Mheshimiwa Spika pia mimi niungane na Waheshimiwa Wenza, kuunga mkono Hoja ya kwamba marehemu Hasmukh Patel almaarufu Mombasa Cement akaweze kupata barabara ambayo itatajwa jina lake maana ni wazi ameweza kugusa maisha ya wanyonge kuanzia masuala ya chakula, masuala ya afya na vile vile pia miundo misingi tumeona mashule ameweza kuweka *perimeter walls* kwa hiyo haya yote naona itakuwa sawia kama wana Mombasa ama Bunge hili likikubali ya kwamba tukaweze kuweka kumbukumbu katika kutaja barabara kwa jina lake. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Hawa Abdulrahman?

Hon. Hawa Abdulrahman: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. I stand to support. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi pia nisimame kuungana na Waheshimiwa wenza kuunga mkono Hoja ilioletwa mbele yetu kwa heshima ya marehemu Hasmukh Patel kuweza kutaja mojawapo ya barabara katika Gatuzi letu kwa heshima aliyotendea wananchi wa Mombasa na Kenya kwa jumla. Mheshimiwa Spika mimi pia ni shuhuda wa yale aliyoyafanya kwa sababu katika Kata ninayo iwakilisha aliweza kunifanyia marekebisho ya madarasa mawili Mheshimiwa Spika kwa mtindo wa kisasa ambayo madarasa hayo yamekuwa yakinawiri zaidi ya yale yaliyopo kwa sababu ya bidii zake lakini pia Mheshimiwa katika yale marekebisho ambayo bwana huyu amekuwa akifanya alikuwa akipenda zaidi kutaja jina Mombasa Cement ambayo Mheshimiwa Spika kimimi ingependeza zaidi kama heshima hii ingebakia kama alivyokuwa akiweka mwenyewe kama alipokuwa akifanya marekebisho ya hospitali, vituo vya polisi kujenga makuta alikuwa akimaliza anaandika jina la Mombasa Cement na hilo ndio liko maarufu kwa wananchi wa Mombasa hii ya Hasmukh Mheshimiwa Spika ni jina lake kama Mkurugenzi lakini wengi wa wananchi hawalitambui moja kwa moja, kwa hivyo hata likiwekwa Hasmukh Patel basi mbele yake kwa mabano aweze...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): There is a Member who is up, what is it?

Hon. Kai: Mheshimiwa Spika hata kidogo naomba kutofautiana na Kiongozi wa Wengi katika swala la kwamba, barabara hii yetu ya Mombasa Cement mwanzo wakati nikizungumza ilikuwa natamani sana kuweka msisitizo huo ya kwamba, isitajwe Mombasa Cement, lakini kwa vile alikuwa nimeona hoja hii haijataja Mombasa Cement, nikaona haina haja nichangie. Namaanisha hivi Kiongozi wa Wengi, Mombasa Cement ni biashara na yeye kama mkuu wa ile biashara alikuwa inampendeza kuona licha kwamba anasaidia, lakini akaweze pia kufanya matangazo ya biashara yake. Lakini mimi naona ni heshima kubwa zaidi tuache biashara kama ilivyo na tukaweze kutaja jina lake ambalo liko katika vile ilivyosajiliwa, ili ikaweze kutambulika ya kwamba, lengo haikuwa ni Mombasa Cement bali lengo ni marehemu ambaye Bwana Hasmukh Patel, japo ni maoni yangu lakini naona itapendeza hivyo zaidi na italeta natija ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Member for the information. Yes, Honourable Athman Mwamwiri?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Wakati mwingine uvumilivu huwa uko na natija kuliko kupurupuka! Mheshimiwa Spika, ni yakini ya kwamba Mkurugenzi wa shirika lile alikuwa akiitwa Hasmukh, lakini yale aliyoyafanya hakuyafanya kwa pesa yake ya mfukoni, aliyafanya kutokamana na mgao wa biashara inayoitwa Mombasa Cement. Ndiposa yeye mwenyewe katika kuyafanya aliyoyafanya Mheshimiwa Spika alikuwa hayatangazi jina lake kwa sababu haikuwa ni mchango wake yeye kama mtu. Mheshimiwa Spika, ninapotumia ofisi ya Bunge hili kutekeleza jambo alafu niandike jina langu itakuwa sijatendea haki Bunge hili, ni iaminike ya kwamba mchango huu umetokana na Bunge hili, haidhuru aliyependekeza hoja hii amesema tumuandike Hasmukh Patel lakini kwa kuwa wananchi hakuna anayetambua kwamba alisaidiwa na Hasmukh Patel, isipokuwa Mombasa Cement. Basi kwa mabano hata kama ni chini ya jina ile, hii Mombasa Cement Mheshimiwa Spika tuiweke kama heshima na kila atakae ona atakumbuka ya kwamba kumbe Hasmukh Patel ndiye aliyekuwa Mkurugenzi wa Mombasa Cement. Kwa sababu pia ile taasisi iliyokuwa ikitoa fungu lile ambalo Hasmukh Patel alikuwa akilisimamia kuyafanya haya lazima sisi kama serikali tuweze kutambua Mheshimiwa Spika, kuweze kuiheshimisha ili iwe mfano, ili iwe ngoa Mheshimiwa Spika kwa tasisi zengine ambazo tuko nazo katika Gatuzi letu, ya kwamba wakiwekeza kwa wananchi serikali ya wananchi ya Mombasa itawakumbuka, itawapatia heshima ya angalau kuwapa jina katika barabara, kwa sababu barabara ni mali ya Kaunti na tuna jukumu ya sisi kupeana jina lile.

Pia Mheshimiwa Spika ingependeza katika aliyeleta hoja hii kutuambia pendekezo la barabara hii, iwe mahali gani kwa sababu tunaweza tukaweka kiwe kibandiko mahali ambapo pengine katika jitihada zake Bwana Hasmukh na Mombasa Cement hawakuwahi kufika kutia mkono lakini kwa kule ambapo waliboresha zaidi kama ndugu yangu Mheshimiwa Madialo anasema wana viwanda katika kata yake. Kwa hivyo wananchi wa pale asilimia kubwa wameajiriwa pale na wanamjua Hasmukh Patel ni nani na wanajua Mombasa Cement ni nini. Mimi katika kata yangu Mheshimiwa Spika nimefaidika nimejengewa madarasa, nimefanyiwa marekebisho na pia wananchi wangu wanajua Mombasa Cement mchango wake ni nini. Kwa hivyo ingependeza Mheshimiwa aliyeleta hoja hii atakapo kuwa anawasilisha atuambie labda pia pendekezo la sehemu makhsusi isije ikapeleka serikali ikapeleka kibandiko cha jina hili katika vitongoji vya Mwakirunge ama vya Shika Adabu ambako pengine kwa siku kunapita pikipiki mbili na baiskeli moja.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 7*

Mheshimiwa Spika itakuwako hatujafanya haki kwa yale makuu ambayo Hasmukh Patel chini ya Mombasa Cement aliweza kutufanyia; nasimama kuunga mkono lakini pia familia yake Mheshimiwa Spika lazima itaarifiwe katika hili waridhie...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): There is a Member up Honourable Madialo! Are you up on a point of order?

Hon. Madialo: On a point of information.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Okay.

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa Spika. Ningependa kumuarifu Kiongozi wa Wengi ya kwamba nilifanikiwa kuwa katika... *let me speak in English; I was in the HBC when this order was being presented and if my memory serves me right the Honourable Speaker requested. In fact it was as if where the road was to be identified was indicated but the Honourable Speaker said that, we should not as an Assembly designate the road because it is not in a purview, we would rather leave it to the executive who will implement this to be the ones to choose where they will honour the departed. Secondly, I would want to correct or seek further clarification from the Leader of Majority, is it in order for him to insinuate that in Shika Adabu there are no vehicles, there are only bicycles. Also, in Mikindani Ward unfortunately we did not benefit as much infrastructural issues with the Mombasa Cement. Infact other Wards and other Constituencies benefitted more that I can tell you for a fact.*

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Juma Mwalimu now that you have been mentioned twice.

Hon. Juma Mwalimu: Mheshimiwa Spika mimi nimesimama na *a point of order* alafu nimuambie pia Kiongozi wa Wengi awache madharau hakuna Wadi ambayo saa hizi imeimarika na imeboreshika kama Wadi ya Shika Adabu. Huko bwana magari ndio kwao lakini saa hii naona amekuja kunidhalilisha na kudhalilisha watu wa Shika Adabu. Kwa hivyo naomba aombe msamaha watu wa Shika Adabu la sivyo hata yeye tutamuwekea mipaka asiende tena Kwale.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Leader of Majority first withdraw that statement.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Mheshimiwa Spika na niombe radhi watu wa Shika Adabu na kufuta kauli hio, lakini Mombasa kama Gatuzi bado ina sehemu ambazo ziko katika mipaka na Gatuzi zengine. Mheshimiwa Spika, nilipotaja Mwakirunge kuna mipaka yake na Kilifi ambayo tunaita aje katika lugha ya kimombo, "No man's land". Katika vitongoji vile Mheshimiwa Spika huduma inayopatikana ni ya kutegea Gatuzi hili na Gatuzi hili kwa hivyo kuimarika kwake sio sawa na kama ni mjini ama vitongoji ambavyo viko upeo wa Wadi. Vilevile Mheshimiwa Spika katika mpaka wetu sisi Mombasa na Kwale tunapakana katika kata ndogo ya Shika Adabu; kuna sehemu kule sisi kama Serikali ya Kaunti ya Mombasa tuliidhinishwa kwa kujengwa shule ya upili na ya msingi. Bwana Spika tukijua ardhi ni yetu lakini ndani ya ardhi yetu Serikali ya Kwale nao walikuja kujenga shule ya chekechea kwa upande wetu wakisema ardhi ni yao.

Sasa unakuta katika kupeleka maendeleo sehemu ile Mheshimiwa si watu wa Kwale si watu wa Mombasa wamekuwa wakitegea na hata barabara bado ni zile zile barabara za mkoloni ambazo hazijatembelewa hata na tinga. Kwa hivyo katika mifano ya vitongoji vilivyoko nje ya maeneo hayo Mheshimiwa Spika ndio nilikuwa nakusudia, ndio inatambulika kuwa ni barabara lakini haitumiki ama haijimarishwa kwa sababu iko katika mpaka. Mheshimiwa Spika, lakini Shika Adabu nimepakana nayo mimi, ni marafiki zangu na mamangu mzazi anaishi katika Wadi ya Shika Adabu siwezi wakosea sana heshima ni ndugu zangu sana na nawapenda na wasininukuu vibaya. Nataka hii iangaziwe ili pia mbeleni Mheshimiwa Spika iko haja ya sehemu zile kuweza kuweka *beacons* ama mipaka ya kusema huku ni kwetu na huduma ziweze kufika katika vitongoji vile.

Nikimalizia Mheshimiwa Spika nilisema kwamba ingependeza pia aliyeleta hoja hii sisi kama Bunge tukipitisha itaarifiwe familia yake ya kwamba wawe na ufahamu Bunge tumeheshimu familia tunataka kupeana jina la barabara ili sije wakaona kibandiko cha jina la mtu wao wakasema tumetumia pasi na ridhaa ya familia. Hilo Mheshimiwa ni pendekezo lakini ninaunga mkono Hoja hii kwa sababu kesho naamini mimi Mungu akijaalia kwa yale ninayo wafanyia watu wa Mombasa pengine mauti yakinikuta itakuwa ni kumbukumbu na Bunge linaweza kuja kwa zama zile ya kwamba tuliweza heshimu mwengine na wao wakaniheshimisha kwa kupeana jina la barabara inayoelekea pale ninapoishi Mheshimiwa Mwamwiri Road. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia. Mheshimiwa Spika kwanza kabisa baada ya kuona hoja hii imeletwa mbele yangu nilikuwa najiuliza huyu Hasmukh Patel Kanji ni nani?! Lakini nimpongeze Kiongozi wa Wengi baada ya kufafanua kwamba huyu Hasmukh Patel Kanji ndiye yule yule *Mombasa Cement*. Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja hii; vilevile pia niombe Waheshimiwa wenza kama tuna mapenzi zaidi ya huyu ndugu yetu ingekuwa bora zaidi pia hata kama itakuwa hiyo Hasmukh Patel Road lakini vilevile pia iwe itakuwa na ufafanuzi kwamba huyu Hasmukh Patel ndio yule yule Mombasa Cement kama vile nilivyotangulia kwanza kwamba nilikuwa ninashindwa kutambua huyu Hasmukh Patel ni nani lakini baada ya kujua nikaona nitasimama kuunga mkono hoja hii. Vilevile Mheshimiwa Spika hakuna kitu kizuri kama tunasema ukizikwa ukiona inakuwa bora vizuri zaidi, tukiona mmoja wetu anatumfanyia mambo mazuri zaidi ambayo yanatupendeza Mheshimiwa Spika pia ni bora zaidi kuweza kumtambua kabla hajakufa kuliko pia tungoje kama amekufa hajui kama kuna nini huko nyuma sisi ndio tuweze kumfanyia hili na lile.

[Applause]

Kwa hiyo kama kuna sababu ya mmoja wetu anatumfanyia mazuri basi tuwe ni wenye kukumbuka kama nikumuweka kwenye barabara awe pia akikaa anapata moyo zaidi ya kufanya yale mazuri kwa sababu atakuwa hajakufa na pia yale mazuri anayaona ambayo amefanyiwa na watu ambayo ni kumaanisha kwamba wanarudisha shukran kutokana na ile kazi nzuri anayoifanya. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii bila ya sababu yoyote ile ya kupinga. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Ibrahim Omondi reply to your Motion?

Hon. Omondi: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, I expected the Honourable Member who has just left the floor to actually give this 100 per cent because I know what Mr. Patel, that is commonly known as Mombasa Cement used to contribute to our community. It resonated well with very many people in Mombasa County. That was even shown when he was being laid to rest, you saw a mammoth crowd who attended the funeral and you could see the emotions that were running down the people. Mr. Speaker, I want to take this particular opportunity to thank the Members who have actually contributed in different ways; you have noted a lot of gaps there. Moving forward Mr. Speaker, next time I think we will be able to factor some of those sentiments when you are putting up such a Motion; so, a good student learns, a good student should not be egocentric...I would like just to say that this is going to be very important to our County because we have adopted this particular Motion. Mr. Speaker this is going to encourage, it's going to motivate even other leaders, other organizations, other directors, they will also be able to actually do exactly what Mr. Patel used to do. Mr. Speaker, as i finish I think as I was running, I was moving this particular Motion I was very categorical and specific because I knew that the word Hasmukh, very many people are not very much aware with it. That is why, in moving my Motion I said that commonly known as Mombasa Cement, Mr. Speaker. So, I expected that Members were keen when I was running my....., I was moving the Motion otherwise Mr. Speaker, thank you very much and may God bless you so much.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Ibrahim Omondi. Honourable Members, I now put the question that the Motion by Honourable Ibrahim Omondi on behalf of Honourable Samir Bhaloo, naming a road in Honour of the late Hasmukh Patel Kanji, be approved by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]

Honourable Members, the Motion on naming road in honor of the late Hasmukh Patel Kanji has been adopted by the House. Yes, Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, the House stands adjourned until Wednesday, 12th March, 2025 at 2:30p.m.

The House rose at 11:00a.m.